# KUITUKUZA QUR_ANI

---

<"xml encoding="UTF-8?>

BISMILAHI RAHMANI RAHIYMI

KWA JINA LA MWENYEEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU

KUITUKUZA QUR_ANI

Walidi bin Mughera alikuwa ni mmoja katika maadui wa kiislamu na Mtume Muhammad -:(s.a.w.w), Siku moja wakati alipokuwa akisikiliza Qur-ani alisema

Qur-ani ni kitabu kizuri kutokana na yaliyomo ndani yake, na ni kitabu chenye kuleta jazba " ,kwa mwanaadamu. Qur-ani ni kitabu bora na hakuna kitabu bora chengine zaidi ya Qur-ani

Maelezo hayo yalimfikia Abu Jahli, na Abu Jahli alikwenda kwa Walidi bin Mughera na -:kumwambia

Kaumu yako imekusanya mali na kukuletea wewe ili uwache kuisifu Qur-ani, mughera alimjibu" -:abu jahli kwa kusema

Mimi nina mali zaidi ya kaumu yangu, na ninajuwa njia za uzungumzaji, kwa hakika maneno" .anayozungumza Muhammad (s.a.w.w.) ambayo yamo katika Qur-ani sio mashairi

:Abu jahli akasema

."Ni lazima utafute njia ili kuiridhisha na kuifurahisha kaumu yako"

Walidi bin Mughera aliomba fursa kwa Abu Jahli ili alifikirie jambo hilo, baada ya kulifikiria :jambo hilo alisema

Huu ni uchawi- yaani Qur-ani ni uchawi, na maelezo yaliyomo humo yametungwa na" mwanaadamu. Walidi bin Mughera aliyasema maneno hayo kutokana na kinyongo alichokuwa nacho moyoni mwake nay eye mwenyewe alielewa wazi kwamba maneno hayo hayana ukweli .(wowote, kwani Qur-ani muujiza utokao kwa Mwenyeezi Mungu (s.w

MUUJIZA WA QUR_ANI

.Moja miongoni mwa miujiza ya Qur-ani ni kwamba Qur-ani imekuja na mtume ambaye umi

Umi ni mtu gani? , katika kipengele hiki hapana budi kuelezea maana ya neno umi ili liweze .kueleweka maana yake

-:Umi ni mtu ambaye hajuwi kusoma wala kuandika, Mwenyeezi Mungu mtukufu anasema

وَمَا كُنتَ تَتْلُو مِن قَبْلِهِ مِن كِتَابٍ وَلاَ تَخُطُّهُ بِيَمِينِكَ إِذاً لاَّرْتَابَ الْمُبْطِلُونَ

Na hakuwa mwenye kusoma kitabu chochote kabla ya hiki, wala hakukiandika kwa mkono .(wako wa kuume (kulia), ingekuwa hivyo wangefanya shaka wale wanaotaka kubadilisha (haki

-:Muujiza mwengine miongoni mwa miujiza ya Qur-ani ni

Ustadh Amiyn Rayhani masiyhi katika barua aliyomuandikia Alameh Sheykh Huseyni Kashif -:Alghataa anasema

Nyinyi mnasema kwamba Qur-ani ni muujiza nah ii ni kauli ya kweli nay a haki, mimi katika kipindi nilichokuwa nikiiishi London na Amerika wakati mwingi nilikuwa nikiisoma Qur-ani kwa lugha hiyo hiyo ya kiarabu, ambapo jambo hilo liliwafanya majirani zangu waingiwe na jazba .pindi niisomapo qur-ani, na waliingiwa na mshawasha akilini mwao kutaka kuijuwa Qur-ani

-:Carbon anasema

Kama kusingelikuwa na miraji, kama Muhammad (s.a.w.w.) hakuwa na tabia nzuri na tukufu, “ na kama Qur-ani haikuwa ikimuongoza mwanaadamu na kumuongowa hakuna shaka kwamba aya zilizomo ndani ya Qur-ani zingelitosheleza kusidikisha Utume wa hadharati Muhammad ”.((s.a.w.w

و بشر عبادى الذين يستمعون القول فيتبعون احسنه

Na wapeni malipo na ujira wale waja wangu ambao huyasikiliza maneno yangu na hufuata njia .bora

Miujiza yote ya Mitume iliyopita ilikuwa ni ya muda na sehemu maalumu, lakini Qur-ani .1 haina muda maalumu, na imeenea katika sehemu na pande zote nne za dunia, na itabakia hadi .milele

.Qur-ani iko hai na itabakia hai kwa kumuongoza mwanaadamu katika njia iliyonyooka .2

Qur-ani inazungumza ukweli na haki, na wala haizungumzi kwa kupendelea upande fulani au .3 .nasaba fulani

MWISHO